Ripoti ya UWABA
Mkutano wa Barabara za Mkoa za Dar es Salaam
12 Mei 2010

Kabla ya mkutano
Mwezi wa kwanza mwaka 2010 wawakilishi saba wa UWABA tulikutana na Meya wa Dar es Salaam, Mhe Adam Kimbisa, ofisini kwake. Kwenye mkutano huu, UWABA tulisema kwamba kuna shida ya ushirikiano kuhusu masuala ya usafiri, hasa usafiri usio wa moto, hapa Dar es Salaam, na kuna mashirika mengi ya serikali (serikali ya jiji, manispaa tatu, Wizara ya Miundombinu, TANROADS, traffic police, DART agency na mengine) pamoja na wafadhili (JICA, World Bank, EU, DANIDA na wengine). UWABA tulipendekeza mkutano (kongamano) wa kila mwezi ambapo mashiriki haya na mengine yakutane na kushirikiana kuhusu sera za usafiri usio wa moto. Mhe Kimbisa alituambia kwamba tayari kuna mkutano kama huu, lakini unahusika na usafiri kwa ujumla na siyo usafiri usio wa moto pekee. Alisema tutaalikwa kwenye mkutano huu ambao unatokea kila baada ya miezi sita, na mkutano ujao utakuwa mwezi wa tano. Hii ilikuwa mara ya kwanza sisi kusikia kuhusu mkutano huu.

Baada ya hapo UWABA tulifuatalia sana ili tupata mwaliko – tuliandika barua kwa mkurugenzi wa jiji ambaye alituambia tufuatalie na Katibu Mkuu wa Mkoa ambaye ni mwenyekiti wa mkutano; tuliandika barua kwake, tulitembelea ofisi za mkoa na tulifuatalia kwa simu mara kwa mara ndani ya miezi mitano ili tupate jibu la barua yetu. Mwishoni tulipata msaada kutoka kwa Ryan Whitney wa Sustainable Cities NGO. Wiki moja kabla ya mkutano tuliwahi kupata majina yetu kwenye orodha ya waalikwa. Tuliruhusiwa kupeleka wawakilishi wawili tu basi UWABA tuliwakilishwa na Elaine Baker-Guni (katibu) na Dominata Rwechungura (mjumbe wa kamati).

Waliohudhuria mkutano
Hatujapata orodha ya wote waliohudhuria mkutano wala hakuna taratibu ya wote kujitambulisha mwanzoni mwa mkutano, lakini tuliona mwenyekiti wa mkutano alikuwa Mkuu wa Mkoa na alisaidiwa na Meya wa Dar es Salaam (Mhe Kimbisa), na wengine waliokuwepo ni Mhe Azzan Zungu Mbunge wa Ilala, Mhe Leonidas Mgamba Mkuu wa Wilaya wa Ilala, ofisa za ofisi ya Mkuu wa Mkoa, wawakilishi wa manispaa zote tatu (wahandisi na wawakilishi wengine), mwakilishi wa DART (Engineer Enock Kitandu), mwakilishi wa TANROADS, mwakilishi wa traffic police, mwakilishi wa SUMATRA, wawakilishi wa TANESCO na DAWASA (kwa sababu miundombinu wa umeme na maji na maji chafu inalingana na miundombinu wa barabara). Kwa hiyo ni nzuri kwamba mashirika haya yanayohusika na usafiri na barabara za mkoa wa Dar es Salaam wanakutana kila mara kwa mara ili kushirikiana. Tunafikiri kwamba UWABA tulikuwa NGO moja pekee yetu kwenye mkutano. Hakuwa na wawakilishi wa wafadhili. Basi inaonekana kwamba mkutano huu zaidi ni mkutano wa mashirika ya serikali.

Baadhi ya waandishi wa habari walialikwa kupiga video ya uzunduzi wa mkutano na tena video ya muhtasari wa mkutano kutoka kwa Mkuu wa Mkoa mwishoni, na ilionyeshwa kwenye TV jioni ile.

Ripoti ya mkutano
Mkutano uliendeshwa kwa lugha ya Kiswahili na wote waliohudhuria walielewa Kiswahili.

Watu wapya kwenye mkutano walipewa nafasi ya kujitambulisha na UWABA tulijitambulisha na tulishukuru Mhe Meya kutupa taarifa kuhusu mkutano huu, na tulikaribishwa kwenye mkutano. Kwa ujumla tulipokelewa vizuri na points zetu zilisikilizwa.

Kulikuwa na document ambayo watu wa kawaida wa mkutano walipewa kuhusu dondoo za mkutano uliopita pamoja na nakala za ripoti zilizoletwa kwenye mkutano huu – UWABA tulipewa lakini wakati mkutano ulimalizika basi tulikuwa na shida kufuatalia baadhi za mazungumzo.

Ajenda kuu ya mkutano ulikuwa kusikiliza ripoti za kifedha kuhusu matumizi ya barabara kutoka kwa TANROADS, manispaa tatu na DART, na kila moja alikuwa ametayarisha ripoti na alisoma muhtasari wakati wa mkutano. Mkuu wa Mkoa alilalamika kwamba ripoti ya TANROADS ilihusika kazi za ofisi ya mkoa ya TANROADS tu na siyo makau makuu ya TANROADS. Pia waliongea kuhusu bajeti ya Ilala ya barabara – Mkuu wa Mkoa alisema kwamba Ilala wanapata mapato makubwa na wachangie zaidi wenyewe na siyo kutegemea serikali kuu.

Maada nyingini zaidi zilizungumziwa wakati wa kusikiliza ripoti, na hapa tumeandika muhtasari. Hapa tumeandika chini ya vichwa mbali mbali na siyo kufuatalia nini ilizungumziwa baada ya nini kwenye mkutano – baadhi za maada zilizungumziwa zaidi ya mara moja wakati wa mkutano.

Maada iliyohusika UWABA / usafiri usiyo wa moto

Umwagiliaji wa maji chafu
Suala la umwagiliaji lilizungumziwa, mfano vifereji mbaya, vifereji vilivyoharibika na taka taka inayoziba vifereji. Mwakilishi wa TANROADS aliomba ushirikiano zaidi kati yao na manispaa kwa sababu mara nyingine hakuna sehemu pa kumwaga maji yanayotoka kwenye barabara.

Zebra na matuta
Kwenye mkutano uliopita waliamua kuweka zebra karibu na ofisi ya Mkuu wa Mkoa barabara ya Kawawa Road Msimbazi Centre ambapo wanafunzi wa shule wanavuka. Walisema waliweka zebra lakini rangi imeshatoka mpaka haionekani. Mhe Azzan Zungu Mbunge wa Ilala alisema kwamba zebra haitoshi na dereva hawafuati, kwamba wanafunzi wapo kwenye hatari kuvuka barabara ya Kawawa, na itabidi kuweka matuta. Mkuu wa Mkoa na mwakilishi wa TANROADS hawakukubali na hiyo walisema matuta yanasababisha msongamano na afadhali iwe zebra tu na askari wawekwe pale. Walikubali kuweka matuta karibu na shule ya Kibada, Mjimwema. Mwakilishi wa TANROADS pia alisema kwamba matuta yanasababisha mashimo kwenye barabara.

Wafanyabiashara wadogo
Waliongea kuhusu kuondoa wafanyabiashara wadogo wadogo kutoka barabara. Pia walizungumza kuhusu shida ya baa kwenye barabara (TANROADS walilalamika).

Mashimo kwenye barabara
Waliongea kuhusu suala la mashimo kwenye barabara, na walisema yanasababisha msongamano. Baadaye, UWABA tulipendekeza tuwe na taratibu ya wananchi kutoa ripoti kuhusu mashimo na hatari zingine barabarani. Mkuu wa Mkoa alisema watoe ripoti kwa kupita serikali za mitaa na pia kwamba mashimo yanajulikana na serikali – shida ni kurekebisha.

DART
Suala la mradi wa DART lilizungumziwa. Mkuu wa Mkoa alisema anataka mkurugenzi wa DART ahudhurie mikutano kama hii na siyo mwakilishi wake tu. Pia alisema kwamba haifai kwamba mradi wa DART inachukua muda mrefu sana kutekelezwa. Mwakilishi wa DART alisema kwamba TANROADS wana jukumu kujenga sehemu ya kwanza kutoka ferry mpaka barabara ya Morogoro, na DART wanasimamia tu. Mkuu wa Mkoa alisema kwamba ni DART wenyewe wana majukumu kufuatalia utekelezaji. Walisema kuna mkutano wa kila mwezi kati ya DART, Benki ya Dunia na TANROADS.

Pia waliongea kuhusu DART phase II na phase III.

UWABA tuliomba kupata reassurance kwamba kweli barabara ya Morogoro itakuwa na njia maalum ya watembea kwa miguu na njia maalum ya baisikeli kama tulivyopata ahadi (kwa sababu ahadi zingine hazijatekelezwa). Mwakilishi wa DART alisema kutakuwa na njia maalum kwa kila aina ya mtumiaji wa barabara – watembea kwa miguu, wapanda baisikeli, mabasi na magari binafsi.

Barabara ya Kigogo-Ubungo
Barabara kutoka Kigogo mpaka Ubungo sasa inajengwa upya na kulikuwa na manzumgumzo kuhusu hiyo mwanzo wa mkutano na pia baadaye. Baadaye UWABA tulilalamika kwamba kwa sasa sehemu za barabara zilizojengwa zina lami ya magari na vifereji tu na hakuna njia ya baisikeli wala hata njia ya watembea kwa miguu – kwa sasa watu wanatembea kwenye lami pamoja na magari yanayoenda kwa kasi. TANROADS walijibu kwamba wana mpango kuweka service roads nje ya vifereji lakini hawajaanza kwa sababu ya taratibu kulipa fidha kwa wenye ardhi.

Barabara kwenda Tegeta
Kuna mpango kuboresha barabara kutoka Mwenge mpaka Tegeta. Waliongea kwamba labda ni bora kuanza Moroco mapaka Tegeta na siyo kuanza Mwenge tu. Mpango ni kuanza mwezi wa kumi. WaJapan wanahusika (JICA ni wadhamini?). Itakuwa na njia nne za magari. UWABA tuliomba michoro ya barabara zipatikani kwa washika dau mapema ili tutoe maoni yetu na kuhakikisha itakuwa na njia za baisikeli na watembea kwa miguu. TANROADS walisema UWABA tufuatalie ofisini kwao.

Mtaa wa Uhuru
Kuna mpango kupanua Mtaa wa Uhuru iwe na njia nne za magari kutoka Msimbazi mpaka Buguruni. Tena, UWABA tuliomba michoro yapatikani na washika dau wasikilizwe maoni yao kabla ya kuanza kujenga.

TAZARA flyover
Walisema kuna mpango kuwa na barabara ya flyover kwenye makutano ya barabara TAZARA.

Barabara za Sam Nujoma na Kilwa
Mkuu wa Mkoa aliuliza kama barabara ya Sam Nujoma imekamilishwa na TANROADS walisema ndiyo imekamilishwa.

UWABA tulisema kwamba tulipata ahadi (kwa maadishi kutoka kwa mkurugenzi wa TANROADS) kwamba barabara za Sam Nujoma na Kilwa Road zitakuwa na njia maalum ya wapanda baisikeli lakini ahadi haijatekelezwa, baadala yake waliweka service roads. Kwa sasa service road ya barabara ya Kilwa ni nyembamba sehemu zingine mpaka wapanda baisikeli wanalazimishwa kutumia barabara kubwa, na service roads ya barabara ya Sam Nujoma inatumiwa na magari kwenda kwa kasi (mtembea kwa miguu aliuwawa kwenye service road ya Sam Nujoma Road na pickup iliyoenda kwa kasi). Tuliomba matuta kwenye service road ya Sam Nujoma kama marekebisho ya shida hii lakini hatujapata jibu. TANROADS walisema shida ya speed ni suala la traffic police.

Parking ya malori na magari kubwa ya mizigo
Mkuu wa Mkoa na wengine walizungumza kuhusu shida ya malori na magari ya mizigo kupaki pande za barabara na kwenye service roads. Mwaklishi wa Traffic police alisema tayari wameanza mradi kukamata magari wanaofanya hivi. Waliongea kuhusu kuwa na sehemu kubwa ya parking ya malori na magari ya mizigo nje ya jiji, mfano Mbezi. Mkuu wa Mkoa alipendekeza sana hiyo, pamoja na kupiga marufuku malori na magari ya mizigo kuja mjini wakati wa asubuhi na jioni ili wafanyakazi wasipate shida kwenda kazini. Pia waliongea kuhusu vipi sehemu za parking kama hizi zinaweza kusanya mapato na kutumikwa na watu wa kuosha gari na fundi za magari. Kuna eneo linalotayarisha Mbezi lakini siyo lakudumu na pia kuna shida folani na bomba za maji zinazozuia njia ya kuingia.

Mikutano ya halmashauri za manispaa
Mkuu wa Mkoa alisema kwamba kuna mikutano za halmashauri za manispaa ni wazi kwa wananchi kuhudhuria. (Hatujapata nafasi kusema ni ngumu kujua mikutano inaendelea siku gani).

Mada zingine zilizozungumziwa
- Mhe Azzan Zungu MP alisema kwamba manispaa ya Ilala wana mapato makubwa lakini wananchi hawaoni matumizi yake, kuna uwezekano kubwa wa kufanya jiji lipendeze bila kuingia gharama kubwa.

- Waliongea kuhusu suala la fidia kwa wenye ardhi. Mkuu wa Wilaya ya Ilala alilalamika kwamba wananchi wanatolewa bila fidia. TANROADS walisema watu hawa walipata onyo wasijenge huko na hawana hati. Pia, haijulikani kwamba road reserve (ambapo ujenzi hauruhusiwi) ina upana gani kwenye maeneo ya jiji na kama ni sawa na upana wa road reserve sehemu za rural areas.
- Suala la kurekebisha mataa yanayoharibika lilizungumziwa.
- Waliongea kuhusu ubora wa ujenzi wa majengo, hasa Kariakoo, na kesi ya jengo moja kudondoka na investigation inayofanyika.
- Mkuu wa Mkoa alifuatalia makubaliano ya nyuma kwamba manispaa watoe taarifa kwa serikali za mitaa kuhusu vibali vya ujenzi vinavyotolewa kwenye maeneo yao.
- Waliongea kuhusu kukusanya mapato zaidi kutoka kwa mabao ya matangazo (billboards)
- Mwakilishi wa TANESCO alisema kwamba kuna mradi kuleta umeme kutoka Gezaulole mpaka Kimbiji. Pia kuna mradi wa Ubungo mpaka Kurasini(?).
- Serikali ya jiji walisema kuna mradi kuhusu madampu ya Mtoni na Pugu.

Mkutano ujao

Hawakuongea kuhusu mkutano ujao kwenye mkutano huu, lakini baada ya mkutano UWABA tulimwuliza Bwana Mungaya ambaye ni ofisa ya mkuu wa mkoa anayehusika na matayarisho ya mikutano hii, na alisema kwamba kutakuwa na mkutano mwingine kati ya Novemba au Disemba. Pia alitushukuru UWABA kwa kuhudhuria na michango yetu ya mawazo.